**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 04** **“Kumsaka Sam”**

**Author:** **Njoki C. Muhoho**

**Medical Advisor** **Dr. Ng’ethe Muhoho**

**Editor** **Maja Braun**

**Kisuaheli** **Eic Ponda**

| Scene | Characters | |
|---|---|---|
| **1** | 1. MAMA SAM<br>2. CHEMU<br>3. MARIA<br>4. DR SALLY<br>5. NARRATOR | **SAM – 17, m.**<br>**MAMA SAM – 40, f.**<br>**MARIA – 43, f.**<br>**EDDI– 36, m.**<br>**DR SALLY – 34, f.**<br>**CHEMU – 15, f.**<br>**GROUP OF STUDENTS – all male**<br>**NARRATOR – m.** |
| **2** | 1. DR SALLY<br>2. MARIA<br>3. CHEMU<br>4. SAM<br>5. NARRATOR | |
| **3** | 1. DR SALLY<br>2. CHEMU<br>3. SAM<br>4. NARRATOR | |

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** **Hujambo na karibu katika sehemu ya nne ya mfululizo wa vipindi Noa "Bongo jenga Maisha Yako" maada kuu tunayoizungumzia ni 'USAFI NA KINGA DHIDI YA UGONJWA WA KUHARA'. Katika makala Iliyotangulia Mtoto Fatu alipoteza maisha yake baada ya kuugua ugonjwa huu. Kakake Sam bado yuaugua nyumbani kwao. Familia hiyo bado inaomboleza kifo cha Ghafla cha Mtoto Fatu. Lakini inalazimika kuondoka Hospitalini haraka ili kuyaokoa maisha ya Sam ambaye ameachwa nyumbani akiwa mahututi. Lazima juhudi za dharura zifanywe kuyaokoa maisha yake dhidi ya ugonjwa huu wa kuhara. Habu tusikilize mambo yatakavyokuwa baada ya familia hiyo kurudi nyumbani ambako jirani yao Maria anawasubiri.**

**SCENE 1: MAMA SAM'S HOME**

**02.** ***SFX: A CAR DRIVES IN. SCREECHES TO A STOP. CAR DOORS OPEN. CAR DOORS BANG SHUT. FOOTSTEPS. DOOR OPENS AND IS SLAMMED SHUT***

**03. MARIA :** **(angry)** Mama Sam! Na binti yangu Chemu, mbona imewachukua muda mrefu hivyo. Mumeniacha peke yangu hapa na Sam,

**04. CHEMU :** ***(calling out)*** Sam, Sam..

**05. MARIA :** (**agitated**) Chemu.. Una nini mtoto wangu?... Eddi na mkeo Sally…. Mbona mnahuzunika?

**06. CHEMU** : ***(distraught)*** Samu samu, Mama …! Sama anakufa ,…..! Sam anakufa…! Usiniache Sam….ohhh Sam uko wapi usiniache..!

**07. MARIA** : ***(angry)*** Chemu… ..Nyamaza ! huna heshima msichana wewe? Kwanini unasukuma watu? uuuuhhh…. Na unakwenda wapi haraka hiyo?

**08. MAMA SAM** : **(crying)** Ooh.. kila Mtu anakufa sasa … ugonjwa wa kuhara utatumaliza… kifo hata mimi nichukue…!!!

**09. *SFX: CHAIR SQUEAKS AND SOMEONE DRAGS IT ALONG A HARD SURFACE.***

**10. MARI** : **Kunaendelea nini hapa? Mtoto Fatu yuko wapi? Au mumemuacha akilala kwenye Gari?.. Najua yeye ni kulia tu na kulala…!**

**11. DR SALLY** ***(interrupts, soberly)*** Maria, Fatu amefariki!

**12. MARIA** : Eti nini ? Dkt Sally unasema nini wewe…? Haiwezekani…ohhh rafiki yangu Mama Sam… Pole sana.. sikujua…Ungenifahamisha mapema….ohhh …hapana…afadhali ningetayarisha ndizi hizi mapema… zingemsaidia. Sasa Fatu ame…..!..

**13. DR SALLY** : Usijilaumu Maria, na hata hizi ndizi hazingemsaidia..!

**14. MAMA SAM** : ***(crying)*** Tufanyeje sasa ....?

**15. NARRATOR** **WAKATI KILA MMOJA ANAPOHUZUNIKA KUFUATIA KIFO CHA FATU CHEMU ANAPATA NAFASI NA KUINGIA CHUMBANI MWA SAM, NA JINSI ALIVYOIKUTA HALI YAKE, HAKUAMINI IKIWA SAM BADO YU HAI..**

**SCENE 2: SAM'S BEDROOM**

16. ***SFX: SOUNDS OF BED CREAKING, RUSTLE OF CLOTHES***

17. **CHEMU :** Sam… Sammuuu… umekufa…? Umekufa…?

18. **SAM :** *(**very weak**)* Ndiyo, Chemu nimekufa.. hali yangu taabani.. ninavyojisikia nitakufa tu ….

19. **CHEMU :** **Tafadhali usiseme hivyo, usiniache Sam...amka ...amka.. lazima twende hospitali .. bila ya kufanya hivyo huu ugonjwa wa kuhara utakuua, kama ulivyomuua mdogo wako Fatu..!**

20. **SAM :** ***(very weak)*** Eti nini ….? Fatu amefariki ... oooh ...hapana.. ..maskini Fatu wetu….!

21. ***SFX: DOOR OPENS. FOOTSTEPS APPROACH***

22. **DR SALLY :** Sam… Umeamka …? Amka, nimekuja kukuchukua nikupeleke Hsopitali. ***PAUSE (softly to herself)*** Ohhh,chumba hiki kinanuka

23. **SAM :** ***(very weak)*** Fatu amefariki Dkt Sally?

24. **DR SALLY :** **Ndio Sam, pole sana Fatu amefariki., lakini cha msingi sasa hivi ni wewe kufika hospitalini haraka iwezekanavyo…**

25. **CHEMU :** **Anajaribu kuamka lakini anashindwa.. hawezi… afya yake imedhoofika sana, hawezi kusimama..!**

26. **SAM** : ***(crying softly)*** Siamini kwamba tumempoteza Fatu.Dkt Sally pia mimi nitakufa? Ninahara vibaya sana, na ugonjwa huu pia utaniua… Sivyo Dkt Sally.?

27. **DR SALLY** : **Iwapo hutapata matibabu haraka, basi uwezo wa kufariki ni mkubwa. Umeugua kwa muda gani?. Na ni lini ulipoanza kuona dalili za ugonjwa huu.. yaani kwenda chooni kila mara..?**

28. **SAM** : **Hata sijui…kama.. tuseme wiki mbili hivi zilizopita…!**

29. **DR SALLY** : **Huo ni muda mrefu sana! Ulipasa kufika hospitalini mara moja. Kuhara ni ugonjwa hatari sana hasa ishara hizo zinapoendelea. Sasa ni lazima twende hospitalini mara moja**.

30. **CHEMU** : Sam, Hukunawa mikono… Ndio sababu unaugua. Nilikuimbia ule wimbo kuhusu umuhimu wa kunawa,… lazima sasa nikufunze…

31. **DR SALLY** : **Lakini si wakati huu Chemu…hebu tumsaidie kumvalisha nguo kisha twende hospitali..!**

32. ***SFX: DOOR OPENS. QUICK FOOTSTEPS APPROACH*.**

33. **MARIA** : **(*disgust)*** Eeehhh, hapa pananuka sana…kama shimo la maji taka…

34. **DR SALLY** : Oh Maria, Afadhali umefika.. Hebu tusaidiane kumvalisha Sam. Hawezi hata kutembea wacha huko kuvaa .!

35. **MARIA** : **Usiniambie nimguse huyu mvulana. tangu mliponiacha amekuwa akihara choo chepesi na kutapika maji tu mchana kutwa…! kama mfereji wa**

**maji taka….!Hata hatujui kama ataendelea kutapika au kuhara. Hebu tazama hizi nguo zake..!**

**36.** ***SFX: RUSTLE OF CLOTHES***

**37. DR SALLY :** ***(urgently)*** **Wacha!!! Wacha..!!! usishike hizi nguo bila kinga… toka nje, toka.. haraka toka ukanawe mikono yako Maria..!**

**38. MARIA :** Mikono yangu ina nini?. Sio mara yangu ya kwanza kuuguza ngonjwa.Nimekuwa nikiwauguza watu wengine!.. Na sioni tofauti yoyote hapa…..!

**39. CHEMU :** Mwalimu anasema ni lazima tunawe mikono kila wakati….

**40. MARIA** ***(interrupting)*** **Msichana …..! kila wakati nakwambia wewe si…..**

**41. DR SALLY :** ***(firmly)*** Maria, Mimi ndiye Daktari hapa.. na nakwambia ukanawe mikono yako vizuri… kisha upesi..! Au sivyo wewe pia utaanza kuu….ulisema nini?... ehhh kutapika na kuhara…! Kama hutanawa mikono yako utaanza kuhara sasa hivi..! Ugonjwa wa kuhara husambaa haraka kwa kushika nguo kama hizi zilizo na kinyesi.Sasa Maria nenda ukanawe mikono yako haraka.

**42. CHEMU** ***(softly raps)***

Osha mikono yako,Osha mikono yako
Mikono safitu,hutumiwa kwa kula
Wasiojali tu,hutumia mikono michafu
Baada ya msala,Osha mikono yako,
Dumisha afya yako,Osha mikono yako

**43.** ***SFX: FOOTSTEPS AWAY. DOOR SLAMS LOUDLY AS CHEMU SINGS***

**44. NARRATOR** WAKATI WANAPOENDELEA KUMSAIDIA SAM KUMPELEKA HOSPITALINI, CHEMU BADO ANAENDELEA KUIMBA WIMBO WAKE KUHUSU KANUNI ZA AFYA, KUMKUMBUSHA KILA MMOJA UMUHIMU WA KUDUMISHA USAFI.MTU ANAPONAWA MIKONO KILA WAKATI ANAWEZA KUJIEPUSHA NA UGONJWA HUU WA KUHARA. KADHALIKA KUJIEPEUSHA KUSHIKA VITU VILIVYOCHAFULIWA NA KINYESI. NI JAMBO LA KUSIKITISHA KUWA MTOTO FATU AMEFARIKI , LAKINI IKIWA JITIHADA ZITACHUKULIWA KUNA MATUMANI KWAMBA AFRIKA ITAFANIKIWA KATIKA VITA DHIDI YA UGONJWA HUU UNAOWAATHIRI WATOTO NA MABAROBARO:.YOTE HAYO YATATEGEMEA IWAPO FAMILIA YA SAM ITAFIKISHA HOSPITALINI KWA WAKATI UFAAO.

**SCENE 3: HOSPITAL WARD**

**45.** ***SFX: HOSPITAL NOISES AND FAR AWAY SOUNDS OF INTERCOMS.***

**46. CHEMU :** Sam, Wamekuweka mpira wa maji kama walivyomfanya Mtoto Fatu…na kisha hakupona..

**47. SAM :** Dr Sally,nashukuru kwa kunileta hospitalini, lakini nina wasiwasi sana. Nahofia kwamba nitakufa kama mdogo wangu Fatu.

**48. CHEMU :** Sam, ukifa hata mimi nafikiri nitakufa tu.

**49. DR SALLY :** Shhh hakuna atakayekufa. Hakuna Mtu anayepaswa kufariki. Mimi na wewe tunaweza kujikinga na ugonjwa huu wa kuhara, na endapo utaambukizwa kwa bahati mbaya tu, na upate tiba mapema, Mtu hupona. Ni rahisi sana.

**50. CHEMU : Najua shangazi Sally Najua…..**

**51. DR SALLY : Ni lazima uwafahamishe wazazi wako, rafiki na kila mmoja umpendaye. Ni rahisi sana kujikinga na ugonjwa huu wa kuhara….. sawa!**

**52. SAM/CHEMU : Ndio Shangazi Sally.**

**53. SAM : Wanafanya nini na chembe chembe za sampuli walizochukua kutoka mwilini mwangu?**

**54. CHEMU ;** ***(cheekily)*** Unahitajika kuweka chembe chembe za kinyesi chako kwenye chupa! Ha ..ha.. ha…!

**55. SAM :** (***embarrassed)*** Aaaahlll mwambie awache shangazi Sally.

**56. DR SALLY :** ***(bemused)*** Ni nini Chemu mwache, mpe nafasi mpenzi wako..

***SAM AND CHEMU TOGETHER*:**

**57. SAM : (*angry)* Si mpenzi wangu**!!!

**58. CHEMU : *(angry)* Si mpenzi wangu** !!

**59. DR SALLY ; *(amused)* Ni vizuri kwamba tumejua ukweli wa mambo kati yenu wawili. Sasa, Sam, tunaweza kuligeukia hili suala la ugonjwa,? hebu tazama sampuli ya kinyesi chako….**

**60. CHEMU : Yuuuk!**

**61. DR SALLY :** ( ***ignoring Chemu)*** Ni maji maji na pia kimechanganyika na chembe chembe za damu na kamasi. Hii ni dalili ya virusi vya amiba..

**62. CHEMU :** Yuuuuuuk!

**63. DR SALLY : Hapa madaktari hufanya uchunguzi kubaini vidudu aina ya Amiba au vimelea vinavyokula sehemu ya ndani ya utumbo wa mwanadamu. Ndicho kilichokisababisha kinyesi kuwa na matone ya damu na kamasi kwenye sampuli hii.Huo ndio ugonjwa wa kuhara damu.**

**64. CHEMU : Yuky yuky… Kuhara…..yuuk!**

**65. DR SALLY : (to Chemu) Ndio Chemu…!, na pia unajihisi mchovu**

**66. SAM : Hii ndio iliyomuua Dadangu Fatu.**?

**67. DR SALLY : Kuna aina nyingi ya vidudu vinavyosababisha ugonjwa wa kuhara damu. Naamini Fatu aliambukizwa vidudu aina ya *Enteropathogenic.***

**68. SAM :** (***interrupts***) ***Entertho***- ni kusema nini ?

**69. DR SALLY :** ***(laughing)*** Nafurahi umerejea katika hali yako ya ucheshi na mchangamfu. Maji uliyotiwa mwilini sasa naona yanaanza kufanya kazi .Hebu sasa nikufafanulie kwa lugha rahisi. Fatu alikuwa akiugua ugonjwa sawa na wako lakini tofauti kidogo tu. Vidudu alivyoambukizwa vilikuwa vikitoa kemikali ambayo iliathiri sehemu ya ndani ya utumbo wake. Hali hii hutatiza uwezo wa mwili kuchuja maji maji na lishe kutoka kwa chakula au maji tumboni

**70. CHEMU :** Maskini Fatu..

**71. DR SALLY :** Aliishiwa na maji kabisa mwilini. Na hii ndiyo inayosababisha vifo miongoni mwa watoto wengi barani Africa Sam.

**72. SAM :** Alilia sana …..?.

**73. DR SALLY :** Hii ni kwasababu , ukosefu wa maji mwilini, husababisha sehemu ya ndani ya utumbo wa mwanadamu kuanza kuliwa pole pole na hatimaye kuleta maumivu mengi tumboni. Wewe umekuwa ukihara sana sivyo.?

**74. SAM :** Ndio kuliko marehemu Fatu.

**75. CHEMU : Yuk!**

**76. DR SALLY : Hasa hii ni kwasababu ya maumivu unayoyasikia yanayosababishwa na msuguano tumboni kutokana na kuongezeka kwa kemikali zinazotoka kwa vidudu hivyo.**

**77. CHEMU : Daktari Sally.. mambo haya sasa yameanza kuwa magumu…vidudu vya *Bacteria,* Amiba na Kemikali aina ya *Toksini?*..**

**78. DR SALLY :** Ohh Pole sana Sam….! Sasa ni wakati wa kumpa nafasi Sam ajimpumzishe. Anahitaji muda mwingi zaidi wa kupumzika ili aweze kupona haraka.

**79. CHEMU :** ***(sulking)*** . Naweze kubaki hapa? Nataka kumuuguza Sam.. lakini sitamsumbua!.

**80. DR SALLY** ***:*** (***laughing***) Chemu, muhimu sasa ni Sam apumzike ili aweze kurejesha nguvu alizopoteza. Tutarudi kumuona kesho.

**81. CHEMU :** (**happy)** Unahakika

**82. DR SALLY :** Kweli kabisa Chemu…!

**83. OUTRO:**

**NARRATOR** Naaam, hatimaye Sam sasa anaendelea kupata nafuu. Madaktari wanafanya kila wawezalo kuhakikisha kuwa afya ya Sam inaimarika baada ya kupewa matibabu ya hali ya juu ya kupambana na vidudu na vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa Kuhara. Kadhalika madaktari hao wanajaribu kumuongezea maji mwilini na dawa za kumuongezea nguvu. Kuna matumaini makubwa ya Sam kupona. Lakini Bado chanzo cha ugonjwa huo hakijajulikana nyumbani kwa Familia ya Mama Sam. Tunafahamu kwamba bado nguo zilizochafuliwa na kinyesi cha Fatu na Sam pia hazijafuliwa.

Je hali hii itamfanya mtu mwengine aambukizwe ugonjwa wa kuhara nyumbani kwa Mama Fatu?

Ungana nasi wakati mwengine kwa makala mengine ya Noa Bongo kuhusu Ugonjwa huu wa Kuhara.

Pia ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki au vinginevyo unaweza kuutazama mtandao wetu wa WWW.DW-WORLD.DE/LBE. PIA USISAHAU KUTUTUMIA MAONI YAKO MSIKILIZAJI. HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.